

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA AFYA

Telegram "AFYA", **DODOMA**  
Namba ya Simu: +255 26 2323267  
Nukushi No: +255 22 2138060  
Barua zote zitumwe kwa **Katibu Mkuu**



Mji wa Serikali – Mtumba,  
Barabara ya Afya,  
S.L.P 743  
**40478, DODOMA**

**28, Januari, 2024,**  
**Dodoma.**

### **TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KATIKA KUADHIMISHA SIKU YA UKOMA DUNIANI.**

**Ndugu Wanahabari;** Leo, Tanzania, inaungana na Ulimwengu mzima katika kuadhimisha Siku ya Ukoma Duniani ambayo huadhimishwa Jumapili ya mwisho wa mwezi wa Januari, ya kila mwaka. Lengo kuu la maadhimisho haya ni kutoa hamasa kwa jamii juu ya wajibu wa kuendelea kupambana na kuutokomeza kabisa Ugonjwa wa Ukoma ifikapo 2030.

**Ndugu Wanahabari;** Ukoma ni ugonjwa sugu ambao husababishwa na bakteria aina ya *Mycobacteria leprae* ambao huambukizwa kwa njia ya hewa na kuzaliana katika mwili wa mwanadamu. Ugonjwa huu hushambulia ngozi na mishipa ya fahamu.

Dalili za ugonjwa wa Ukoma ni pamoja na mabaka yenye rangi ya shaba mwilini ambayo hayaumi wala hayawashi bali hupoteza hisia unapoyagusa na yanaweza kujitokeza mahala popote mwilini, kuanzia kichwani hadi miguuni. Ugonjwa huu unaweza kusababisha ulemavu wa kudumu ikiwa ni pamoja na vidonda sugu mikononi na miguuni, kukakamaa viungo, kuharibu sura ya mtu, kukatika viungo na upofu

**Ndugu Wanahabari;** Maadhimisho ya mwaka huu yamebeba kauli mbiu isemayo "**Thamini Utu; Tokomeza Unyanyapaa dhidi ya Waathirika wa Ukoma**". Kaulimbiu hii inachagiza umuhimu wa kila Mtanzania kushiriki katika kutokomeza ugonjwa huu. Ugonjwa wa Ukoma si ugonjwa wa kulogwa, kurithi, wala laana, ni ugonjwa wa kuambukizwa, unatibika na kupona. Hivyo naisihi jamii kuachana kabisa na dhana hizo potofu na aina zote za unyanyapaa.

Tunafanya maadhimisho ya mwaka huu huku tukishuhudia kupungua kwa kiwango cha wagonjwa wa Ukoma hapa nchini Tanzania. Idadi ya wagonjwa wapya imepungua kutoka wagonjwa 2,297 mwaka 2015 hadi wagonjwa 1,309 mwaka 2023 sawa na punguzo la asilimia 57. Kwa tafsiri hii, mwaka 2023 nchi yetu ilikuwa na wagonjwa 3 kwa kila watu 100,000 hivyo, Tanzania imefika kiwango cha awali cha shirika la Afya Duniani cha kutokomeza ugonjwa wa Ukoma yaani chini ya mgonjwa mmoja kati ya watu 10,000 tangu mwaka 2006.

**Ndugu Wanahabari;** Pamoja na mafanikio hayo, bado kuna halmashauri 19 katika Mikoa ya **Morogoro, Lindi, Dar es Salaam, Mtwara, Kigoma, Tanga, Dodoma, Geita, na Pwani** ambayo haijafikia viwango vya utokomezaji. Tunao wajibu wa

kuendelea na mapambano ili kutokomeza Ukoma katika Mikoa hiyo. Hivyo napenda kutoa rai katika maeneo yafuatayo:

1. Kila mwanajamii kutambua dalili za Ukoma na kuhakikisha wote wenye dalili wanafika katika kituo chochote cha kutolea huduma za afya kwa uchunguzi na matibabu.
2. Waganga Wakuu wa Mikoa na Halmashauri, kushirikiana na Vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini kuhakikisha wanafanya uchunguzi wa Ugonjwa wa Ukoma katika kaya zote zenye wagonjwa wapya wa Ukoma na kutoa tiba kinga.
3. Kila Halmashauri nchini kuhakikisha; inafanya juhudi kuibua wagonjwa, inafuatilia mwenendo wa ugonjwa, na kuwa na takwimu sahihi za kufuatilia wagonjwa kulingana na maeneo au vijiji au mitaa wanakopatikana.

**Ndugu Wanahabari;** Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wadau wote wa ndani na nje ya nchi wanaoendelea kuunga mkono juhudi za Serikali katika kutokomeza ugonjwa wa Ukoma nchini. Aidha, nawapongeza wanahabari kwa kuendelea kuelimisha jamii kuhusu masuala ya afya hususan ugonjwa wa Ukoma.

Mwisho, Napenda kuwahakikishia ya kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** itaendelea kuboresha huduma za afya nchini ili kufikia malengo ya kitaifa na kimataifa.

***NI WAJIBU WETU "KUTHAMINI UTU NA KUTOKOMEZA UNYANYAPAA DHIDI YA WAATHIRIKA WA UKOMA HAPA NCHINI"***



Prof. Tumaini J. Nagu

**MGANGA MKUU WA SERIKALI**